BARAZA LA WAWAKILISHI – ZANZIBAR

ORODHA YA SHUGHULI ZA LEO

# BARAZA LA KUMI NA MOJA LA WAWAKILISHI

## MKUTANO WA TATU

**Kikao cha Nane – Tarehe 14 Mei, 2026**
Kikao Kitaanza Saa 3.00 (Tatu) Asubuhi
na Dua Zitasomwa.

## I. HATI ZA KUWASILISHA MEZANI:

**Waziri wa Kazi na Uwekezaji:**

Hotuba ya Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Kazi na Uwekezaji kwa mwaka 2026/2027.

**Mwenyekiti wa Kamati ya Uchumi na Uwekezaji:**

Hotuba ya Maoni ya Kamati ya Uchumi na Uwekezaji kuhusu Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Kazi na Uwekezaji kwa mwaka 2026/2027.

## II. MASWALI:

**Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais, Sera, Uratibu na Baraza la Wawakilishi:**

335. MHESHIMIWA ABDULWAHAB SAID ABUBAKAR (Jimbo la Chake Chake) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais, Sera, Uratibu na Baraza la Wawakilishi:

Tafiti za kitaaluma na zisizo za kitaaluma ni nyenzo muhimu katika kuisaidia Serikali kufanya maamuzi sahihi ya kisera na maendeleo. Kwa mujibu wa taratibu zilizopo, watafiti hupewa vibali vya kufanya tafiti zao Zanzibar na hutakiwa kuwasilisha nakala za tafiti zao baada ya kukamilika.

(a) Ni tafiti ngapi zimetolewa vibali na kufanywa Zanzibar katika kipindi cha miaka mitano (2020-2025).

(b) Je, matokeo na mapendekezo ya tafiti hizo yanatumika vipi katika kuimarisha sera, mipango na maamuzi ya Serikali.

(c) Je, kuna utaratibu gani wa kufuatilia uwasilishaji wa nakala za tafiti, hususani zile zinazofanywa na wageni.

<u>Ofisi ya Makamu wa Kwanza wa Rais</u>:

482. MHESHIMIWA KOMBO MWINYI SHEHE (Jimbo la Wingwi) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Kwanza wa Rais:

Serikali inaendelea kutekeleza miradi mbalimbali katika maeneo tofauti mijini na vijijini, ili kuweza kuwafikishia wananchi wake huduma bora.

(a) Je, ni kwa kiasi gani Serikali inazingatia miradi hiyo kimazingira.

(b) Je, Serikali inafanya utafiti wa kina wa kimazingira kabla ya miradi husika kuanza.

<u>Wizara ya Fedha na Mipango:</u>

11. MHESHIMIWA BAKAR HAMAD BAKAR (Jimbo la Wawi) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Fedha na Mipango:

Ni kawaida kwa Serikali kulipa fidia kwa wananchi pale inapobidi kufanya hivyo, ili kuweza kutekeleza miradi mbalimbali ya maendeleo.

Je, ni vigezo gani vinavyotumika katika kufanya tathmini ya thamani ya mali za wananchi zinazotakiwa kulipwa fidia.

<u>Wizara ya Ujenzi na Uchukuzi:</u>

13. MHESHIMIWA MOHAMMED ALI SALIM (Jimbo la Ziwani) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Ujenzi na Uchukuzi:

Kumekuwa na changamoto ya kuingia na kutoka katika Bandari ya Mkoani, kutokana na abiria kuzuiwa kuingia na usafiri wao binafsi na hata usafiri wa umma. Hali hii inawapelekea abiria hao kupata

usumbufu wa kutembea masafa marefu kutoka maeneo wanayoteremka gari hadi bandarini.

Je, ni sababu gani za msingi zinazopelekea abiria kuteremka na kutembea masafa marefu kufika bandarini.

27. MHESHIMIWA ABDULWAHAB SAID ABUBAKAR (Jimbo la Chake Chake) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Ujenzi na Uchukuzi:

Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar inaendelea kutekeleza miradi ya ujenzi na kuimarisha madaraja ya kihistoria pamoja na ujenzi wa madaraja mapya katika maeneo mbalimbali ya nchi, kwa lengo la kuimarisha miundombinu ya usafiri na kuhakikisha muunganiko wa kijamii na kiuchumi katika maeneo mbalimbali.

Je, ni lini Serikali italijenga Daraja la Tinga Tinga linalounganisha kijiji cha Tibirinzi, Chake Chake na Kisiwani, ili kurahisisha usafiri wa wananchi, kuongeza usalama na kuimarisha shughuli za kijamii na kiuchumi katika maeneo hayo.

## <u>Wizara ya Ardhi na Maendeleo ya Makaazi:</u>

269. MHESHIMIWA SHAFI MOHAMMED SHAFI (Jimbo la Wete) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Ardhi na Maendeleo ya Makaazi:

Miongoni mwa neema ambazo Rais wa Kwanza wa Zanzibar, Hayati Abeid Amani Karume, amewaachia wananchi wa Zanzibar, ni kuwajengea nyumba maarufu zinazojulikana kwa jina la Nyumba za Mchenzani ambazo zimejengwa Unguja na Pemba. Kwa bahati nzuri Wilaya ya Wete ilibahatika kujengwa nyumba hizo katika jimbo la Wete katika maeneo ya Mtemani. Hata hivyo, tangu kujengwa kwake hadi leo, hazijawahi kufanyiwa ukarabati na sasa miundombinu yake ya maji machafu yote imekuwa chakavu na hatarishi.

(a) Je, ni lini Serikali itazifanyia matengenezo nyumba hizo.

(b) Je, Serikali ina kauli gani juu ya usalama wa maisha ya wananchi wa jimbo la Wete wanaoishi kwenye nyumba hizo.

**Wizara ya Kilimo, Umwagiliaji, Maliasili na Mifugo:**

47. MHESHIMIWA JAKU HASHIM AYOUB (Jimbo la Paje) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Kilimo, Umwagiliaji, Maliasili na Mifugo:

Wakala wa Matrekta Zanzibar ni taasisi ya umma iliyoanzishwa kwa Sheria namba 2 ya mwaka 2019, iliyopitishwa na Baraza la Wawakilishi tarehe 07 Februari, 2019. Hata hivyo, hivi sasa inasemekana Wakala huu imeunganishwa na Karakana.

(a) Je, kwa kuwa Wakala wa Matrekta umeanzishwa kwa Sheria, kama umeunganishwa na taasisi nyengine ni kwa Sheria gani iliyotumika.

(b) Kama Wakala wa Marekta umeunganishwa bila ya kufanyika mabadiliko ya Sheria, kwa kiasi gani Wizara inaikiuka Sheria ya Wakala iliyotungwa na Baraza la Wawakilishi.

(c) Je, kuna tathmini gani imefanyika kubaini kama kuunganishwa kwa Wakala wa Matrekta na Karakana kunaweza kuleta ufanisi, tija na wepesi ule ule wa kuwahudumia wakulima.

**Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali:**

102. MHESHIMIWA JAKU HASHIM AYOUB (Jimbo la Paje) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali:

Hivi karibuni Baraza la Mitihani la Tanzania (NECTA), lilitoa matokeo ya mitihani ya Kidato cha Nne kwa Tanzania. Skuli kadhaa zimefanya vizuri kwa upande wa Zanzibar, hata hivyo zipo baadhi ya skuli hazikupata matokeo ya kuridhisha.

(a) Je, ni skuli gani kumi na tano kwa upande wa Unguja na kumi na tano kwa upande wa Pemba ambazo zimefanya vibaya katika mitihani hiyo.

(b) Ili kuimarisha ufaulu wa skuli hizo na changamoto hiyo isijirudie tena, Je, ni hatua gani Wizara imezichukuwa.

481. MHESHIMIWA KOMBO MWINYI SHEHE (Jimbo la Wingwi) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali:

Skuli ya Sekondari Chwaka Tumbe ni ya Mchipuo na bado ina changamoto ya mrundikano mkubwa wa wanafunzi kwenye bweni la wanawake.

(a) Je, Serikali inalifahamu vipi tatizo hili.

(b) Je, ni upi mpango wa dharura wa kuliondoa tatizo hili.

**Wizara ya Maji, Nishati na Madini:**

288. MHESHIMIWA ALLEY MASOUD ALLEY (Jimbo la Mtambile) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Maji, Nishati na Madini:

Pamoja na ahadi ya Serikali kupitia Wizara yako ya kusambaza maji kwa kutumia magari maalum hasa katika maeneo ambayo wananchi wanakosa maji hayo, hadi sasa katika jimbo la Mtambile bado ahadi hiyo haijatekelezwa, huku wananchi wa jimbo hilo wanaendelea kupata usumbufu.

Je, Serikali inalichukulia kwa uzito gani suala hili, hasa ikizingatiwa kwamba kina mama ndio wanaoteseka zaidi.

**Wizara ya Habari, Sanaa, Utamaduni na Michezo:**

375. MHESHIMIWA MAKAME MOHAMED SUFIANI (Jimbo la Chumbuni) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Habari, Sanaa, Utamaduni na Michezo:

Serikali imejenga viwanja vingi vya michezo vyenye hadhi ya kitaifa na kimataifa vikiwemo vya Wilaya.

Je, viwanja hivyo vinasimamiwa na nani.

**Wizara ya Mawasiliano, Teknolojia na Habari ya Ubunifu:**

243. MHESHIMIWA ABDULGHANI ISMAIL ZUBEIR (Jimbo la Malindi) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Mawasiliano, Teknolojia ya Habari na Ubunifu:

Serikali imekuwa na jitihada madhubuti ya kuziba pengo la kidijitali Zanzibar, kwa kutandaza Mkonga wa Taifa, kuongeza upatikanaji wa huduma za Serikali mtandaoni na upatikanaji wa *Internet*.

(a) Je, Wizara ina idara, taasisi au kituo chochote cha Taifa cha uangalizi wa usalama wa mtandao (Cyber Security).

(b) Kwa nini Wizara haina idara, taasisi au kamisheni inayoshuhulikia mageuzi na taaluma ya *ICT* kitaifa, pamoja na ubunifu wa kidijitali*,* kiviwanda na uwekezaji.

**Ofisi ya Rais, Katiba, Sheria, Utumishi na Utawala Bora:**

49. MHESHIMIWA SEIF HAMAD SULEIMAN (Jimbo la Ole) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Katiba, Sheria, Utumishi na Utawala Bora:

Mfumo wa Elimu ya Tanzania umebadilika kutoka '*Knowledge Based'* kwenda '*Competence Based'*, ambao humpa maarifa zaidi mwanafunzi ya kuweza kutekeleza majukumu yake kwa uweledi na ufanisi zaidi atakapokuwa mtumishi wa Serikali.

Je, ni lini Serikali itafanya marekebisho ya Mfumo wa Utumishi ili kutambua mfumo wa *National Technical Awards* (NTA) ambao unatokana na '*Competence Based System'.*

**Wizara ya Afya:**

36. MHESHIMIWA JAKU HASHIM AYOUB (Jimbo la Paje) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Afya:

Kwa kuwa Hospitali ya Mnazi Mmoja inaendelea na matengenezo, watendaji wake wengi wamehamishiwa katika hospital nyengine. Hata hivyo, kumekuwa na malalamiko kuhusu ugawaji wa watumishi hao kuwa, wale wenye sifa hawatakiwi Hospitali ya Lumumba na badala yake wamepelekwa Hospitali ya Pangatupu na baadhi ambao hawana sifa za kutosha wamechukuliwa. Mfano wenye stashahada wamewekwa Lumumba na wenye shahada ya pili wamepelekwa Pangatupu.

(a) Je, sababu gani zimepelekea ugawaji wa namna hiyo.

(b) Je, hatua gani zitachukuliwa kurekebisha changamoto hiyo.

56. MHESHIMIWA ABDULGHAN ISMAIL ZUBEIR (Jimbo la Malindi) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Afya:

Katika kuimarisha huduma za afya, Serikali imeamua kuingia mikataba na baadhi ya wawekezaji ili kuendesha na kusimamia utoaji wa huduma katika hospitali zetu.

(a) Je, Serikali inachukua juhudi gani kudhibiti mifumo ya sekta ya afya inayoendeshwa na wawekezaji katika hospitali hizi.

(b) Je, kwa kiasi gani mifumo ya sekta ya afya inayoendeshwa na wawekezaji inakaguliwa na kufuatiliwa na taasisi kama za Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali, E-Government na ZAECA.

(c) Kwa kiasi gani ukaguzi wa mifumo hiyo unazingatiwa katika uhakiki wa kusomana kwa taarifa, ili kuzuia uwezekano wa kuwepo uchezeaji wa mifumo kwa lengo la kupotosha taarifa.

## III. HOJA ZA SERIKALI:

**Waziri wa Kazi na Uwekezaji:**

Kwamba Baraza hili lijadili Makusudio na Shabaha zilizomo katika Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Kazi na Uwekezaji kwa mwaka 2026/2027.

Zanzibar,
14 Mei, 2026.

(Raya Issa Msellem)
KATIBU WA BARAZA LA
WAWAKILISHI, ZANZIBAR